



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:**

(Tangazo hili limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo jumla ya Tsh. 1,468,676,159.53 zimetengwa hadi kufikia Septemba 30. Hivyo, vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kinachotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
- iii. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya Wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha Watu Wenye Ulemavu kiwe na Wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu Mwenye Ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya manajimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu na kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kijasiriamali; na
- v. Wanakikundi lazima wawe raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tembelea **tovuti: [mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz](http://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz)**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:

- Barua ya kikundi kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa
- Muhtsari wa kikundi wa kuomba mkopo
- Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo
- Taarifa ya akaunti ya bank (Bank statement ya akaunti ya kikundi)

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 30 mwezi 10 mwaka 2024.

Tangazo hili limetolewa na:-

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.